JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA PILI

28 OKTOBA, 2026

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA PILI – TAREHE 28 OKTOBA, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

20. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini fedha za kumalizia ujenzi wa Zahanati za Vijiji vya Nyashimba, Funika, Mandela, Nhelela, Kidema na Igwata zitapelekwa.

21. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (TEMEKE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Bweni la Wavulana katika Shule ya Sekondari Kibasila katika Halmashauri ya Temeke.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

22. MHESHIMIWA ASHA JUMA KOMBO (MFENESINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inachakata Pamba na kuuza bidhaa za Pamba badala ya kuuza Pamba ghafi nje ya nchi.

WIZARA YA NISHATI:

23. MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (KARAGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, kwanini maeneo ya Mamlaka ya Mji wa Kayanga na Omurushaka ambayo kiuhalisia ni Vijiji gharama za umeme ni Shilingi 320,000/= badala ya 27,000/=.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

24. MHESHIMIWA JOHN STEPHANO LUHENDE (BUKENE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha VETA katika Jimbo la Bukene ili kuwasaidia Vijana kujiajiri.

25. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABBAS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio ya masharti ya usajili wa Shule Binafsi nchini.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

26. MHESHIMIWA JOHN FRANCISCO NZILANYINGI (NYAMAGANA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukopesha mtu mmoja mmoja na vikundi vya uchuuzi wa Samaki katika Mialo ya Jiji la Mwanza.

WIZARA YA MAJI:

27. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza Dira ya Taifa ya 2050 kwa kila mkazi wa Mkoa wa Katavi kupata huduma ya maji nyumbani kwake.

28. MHESHIMIWA DEVOTHA DANIEL MBURARUGABA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Miradi ya Maji inakamilika Wilayani Kyerwa hususani Kata ya Nkwenda, Kaisho na Isingiro.

WIZARA YA MADINI:

29. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, kuna Sera ya kulazimisha *Technology Transfer Agreements* kwenye Miradi ya *Critical Minerals*.

WIZARA YA UJENZI:

30. MHESHIMIWA MARY DANIEL SURATI (SERENGETI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Natta – Mugumu kwa kiwango cha lami utaanza.

31. MHESHIMIWA ONESMO MERDSON MNKONDYA (MBOZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itamlipa Mkandarasi malipo ya awali ya ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba yenye Kilometa 130.

WIZARA YA AFYA:

32. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha ujenzi wa Wodi ya Wanawake katika Hospitali ya Mkoa wa Songwe unakamilika kwa asilimia mia moja.

WIZARA YA KILIMO:

33. MHESHIMIWA ZUBERI YAHYA MFAUME (MOROGORO KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wakulima wa Karafuu kwa kuwapa elimu, mbegu bora na mikopo ya pembejeo ili kuongeza uzalishaji.

34. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatoa elimu kwa Wakulima wa Tumbaku Tabora kuhusu matumizi ya Nishati safi ya kukaushia Tumbaku.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

35. MHESHIMIWA YOHANA STEPHEN MSITA (ITIGI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti Wanyama waharibifu hususani Tembo wanaosababisha uharibifu wa mazao na mali Jimbo la Itigi.

III. KAMATI YA MIPANGO:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

DODOMA **BARAKA I. LEONARD**
28 OKTOBA, 2026 **KATIBU WA BUNGE**